# 14- Ihraam

## 1-Maana ya Ihraam

Maana ya Ihraam kilugha: ni haraam, yaani ni jambo lililoharamishwa.

Kiistilahi: Ni kuweka niyyah ya kuingia katika 'ibaadah ya Hajj au 'Umrah; kwa maana mtu anapoazimia kutekeleza 'Umrah au Hajj akaanza taratibu zake *Miyqaat* na kutamka *Talbiyah*, huwa ameshaingia katika Ihraam na kwa hivyo kuna baadhi ya vitendo huwa ni haraam kwake kuvitenda, hadi atakapojitengua na Ihraam.

Muislamu anapoazimia kufanya 'Umrah au Hajj lazima ahirimu kabla ya kuvuka '*Miyqaat*.' Kwani hapa ndipo panapoanzia taratibu za 'Umrah na Hajj. Kufanya ghuslu na kuvaa nguo pekee haimaanishi kwamba mtu ameshaingia katika Ihraam, na ingawa shuka mbili zinaitwa 'Ihraam' lakini sharti ya kuingia Ihraam ni lazima ahirimu *Miyqaat*. Anayeingia katika Ihraam huitwa 'Muhrim'.

Wanaosafiri kwa gari wakataka kuingia Makkah, lazima wasimame *Miyqaat* zao ikitegemea nchi wanazotokea. Wanaosafiri kwa ndege kufikia Makkah kupitia Jeddah kutekeleza 'Umrah kwanza kabla ya kwenda Madiynah, wanahirimia ndani ya ndege. Kwa hiyo wanatakiwa wajitayarishe kuingia katika Ihraam kufanya *ghuslu* kabisa tokea nyumbani. Wanawake wavae nguo zao nyumbani. Wanaume huvaa katika ndege wakipenda au huvaa kabisa tokea nyumbani. Kawaida inatangazwa kwenye ndege inapokaribia *Miyqaat*. Ni vyema wanaume waharakize kuvaa shuka zao za Ihraam na pia kutia niyyah moyoni kabisa kwani huenda ikawapita *Miyqaat* bila ya kujua, jambo litakalokalifisha kulipa *kaffaarah* hapo Makkah. Itambulike kwamba ni makosa kutokuhirimia kabla ya Miyqaat ukashuka kiwanjani bila ya kuhirimia au hadi ukafika Makkah. Ukifanya kosa hili, basi inakupasa kurudi *Miyqaat* ili uingie katika Ihraam, na ukishindwa, basi hukmu yake itakuwa ni utoe fidia ya kuchinja mnyama ukifika Makkah na uwagawie masikini wa Makkah na wala huruhusiwi kumla mnyama huyo wala kuwapa matajiri kwa kuwa ni mnyama wa *kaffaarah* ambaye anatakikana aliwe na masikini tu.

## Kujitayarisha Kabla Ya Kuingia Katika Ihraam

- Kukata kucha zote.
- Kunyoa nywele za kwapani na sehemu za siri.
- Kuchana nywele vizuri ili zisitoke nyingi unapofanya ghuslu.
- Kukata, kupunguza masharubu. Ndevu ziachwe bila ya kukatwa au kupunguzwa.
- Kununua nguo za Ihraam mapema. Ni vyema kuchagua iliyo nzito na si nyepesi kwani inapokuwa joto, hutokwa majasho na kuganda mwilini.
- Wanawake kutumia sabuni, shampoo isiyo na manukato.
- Wanaume kufanya mazoezi ya kuvaa Ihraam na kutembea kidogo ili ahakikishe ameijulia kuivaa isije ikamvuka.
- Ikiwa ni msafiri kwa gari, kuwa na mfuko wa kutilia nguo za Ihraam, sabuni, shampoo na unavyohitaji katika kufanya *ghuslu*. Vyote hivi vitakuwa kwenye begi la mkononi.

**2-Kuoga na kuingia katika Ihraam**

Ukiwa nyumbani au *Miyqaat*, fanya ghuslu, kisha jitie manukato (wanaume pekee). Vaa nguo zako. Wanawake wavae nguo zozote zinazotimiza masharti ya hijaab. Wanawake hawatakiwi kujitia manukato yoyote.

**3-Namna Ya Kuivaa Ihraam kwa Mwanamme**

Shuka mbili nyeupe zinazozouzwa tayari. Unaweza kununua mapema kabla ya kusafiri katika nchi yako au pia zinauzwa katika maduka pembezoni ya *Miyqaat*.

Shuka moja inafungwa kiunoni. Inaruhusiwa kuvaa mkanda wa kuwekea pesa kusaidia kuikaza vizuri shuka. Ya pili inatupwa kufunika mabega yote.

Unapoanza kufanya *Twawaaf* unatakiwa uivae kama inavyojulikana kuwa ni '*Idhwtwibaa'* kuwa utafungua upande wa bega la kulia liwe wazi.

**4-Yanayoruhusiwa kuvaa**

Saa, miwani ya macho na ya jua, lenzi ya jicho, viatu, kanda mbili, makubadhi visivyofunika vifundo vya mguu.

**5-Vazi La Ihraam kwa Mwanamke**

Kishariy'ah hakuna vazi maalum kwa mwanamke, bali anatakiwa avae vazi linalotimiza hijaab kishariy'ah.

**6- *Talbiyah***

Baada ya kwishatiya niyyah moyoni, ambayo pia imeshaaingia moyoni tokea ulipoazimia safari ya 'Umrah au ya Hajj, inapendekezeka kuanza *Talbiyah* kwa kumuitikia Allaah (سبحانه وتعالى) kwa kutaja aina ya Hajj au Umrah unayoitekeleza kama alivyofanya Rasuli (صلى الله عليه وآله وسلم):

عن بَكرِ بنِ عبدِ اللَّهِ المزنيِّ ، قالَ سمعتُ أنسًا ، يحدِّثُ قالَ : سَمعتُ النَّبيَّ صلَّى اللهُ عليْهِ وسلَّمَ يلبِّي بالعمرةِ والحجِّ جميعًا ، فحدَّثتُ بذلِكَ ابنَ عمرَ فقالَ : لبَّى بالحجِّ وحدَه ، فلقيتُ أنسًا فحدَّثتُهُ ، بقولِ ابنِ عمرَ فقالَ أنسٌ : ما تعدُّونا إلَّا صِبيانًا ، سمعتُ رسولَ اللَّهِ صلَّى اللهُ عليْهِ وسلَّمَ يقولُ: ((لبَّيْكَ عُمرةً ، وحَجًّا)) معًا

Imepokelewa toka kwa Bakr bin 'Abdillaah Al-Muzniyy ambaye amesema: "Nilimsikia Anas akihadithia: Nimesikia Nabiy (صلى الله عليه وآله وسلم) akitamka *Talbiyah* ya 'Umrah na Hajj kwa pamoja. Nikamhadithia hayo ibn 'Umar". Akasema: "Akatamka *Talbiyah* ya Hajj pekee. Nikakutana na 'Anas nikamhadithia kuhusu kauli ya Ibn 'Umar. Akasema Anas: 'Mnatufanya

kama watoto' nimemsikia Rasuli wa Allaah (صلى الله عليه وآله وسلم) akisema: ***((Labbayka-'Umratan wa Hajjaa)***)[1]

| 'Umrah au aina ya Hajj | *Talbiyah* | Matamashi na maana |
|---|---|---|
| 'Umrah pekee au 'Umrah ya Hajj *At-Tamattu'* | لَبَّيْكَ اللَّهُمَّ عُمْرَة | ***Labbayka-Allaahumma 'Umrah***<br><br>Ee Allaah naitikia kutekeleza 'Umrah. |
| Tarehe 8 utakapokwenda *Minaa* au ikiwa ni Hajj Ya *Al-Ifraad* | لَبَّيْكَ اللَّهُمَّ حَجًّا | ***Labbayka-Allaahumma Hajjaa***<br><br>Ee Allaah naitikia kutekeleza Hajj. |
| Hajj na 'Umrah pamoja (*Al-Qiraan*) | لَبَّيْكَ اللَّهُمَّ عُمْرَةً وَحجًّا | ***Labbayka-Allaahumma 'Umrah wa Hajjaa***<br><br>Ee Allaah naitikia kutekeleza 'Umrah na Hajj. |

Ikiwa unamfanyia mtu 'Umrah au Hajj umtaje jina lake useme kama hivyo ila umalizie:

لَبَّيْكَ اللَّهُمَّ حَجًّا عَنْ فُلاَنِ بِنْ فُلاَنِ

***Labbayka-Allaahumma Hajjaa 'an fulaan bin fulaan***

[1] Muslim, Swahiyh Ibn Maajah, Swahiyh Abu Daawuwd, Swahiyh An-Nasaaiy.

Fadhila za *Talbiyah:*

عَنْ سَهْلِ بْنِ سَعْدٍ قَالَ: قَالَ رَسُولُ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ: **((مَا مِنْ مُسْلِمٍ يُلَبِّي إِلَّا لَبَّى مَنْ عَنْ يَمِينِهِ أَوْ عَنْ شِمَالِهِ مِنْ حَجَرٍ أَوْ شَجَرٍ أَوْ مَدَرٍ حَتَّى تَنْقَطِعَ الْأَرْضُ مِنْ هَاهُنَا وَهَاهُنَا))**

Imepokelewa toka kwa Sahl bin Sa'd amesema: Rasuli wa Allaah (صلى الله عليه وآله وسلم) amesema: ***((Hakuna Muislamu yeyote anayetamka Talbiyah, isipokuwa kila kilokuweko kuliani au kushotoni kwake; ikiwa ni kutokana na jiwe au mti au udongo vinasoma pamoja naye mpaka ardhi inapoishia huku na kule [kuliani kwake na kushotoni kwake]***))[2]

Kisha endelea kutamka *Talbiyah*

**لَبَّيْكَ اللَّهُمَّ لَبَّيْكَ, لَبَّيْكَ لاَ شَرِيكَ لَكَ لَبَّيْكَ, إِنَّ الْحَمْدَ, وَالنِّعْمَةَ, لَكَ وَالْمُلْكَ, لاَ شَرِيكَ لَكَ**

***Labbayka-Allaahumma Labbayk. Labbayka laa shariyka Laka Labbayk. Innal-Hamda Wan-Ni'imata Laka wal-Mulk laa shariyka Lak.***

"Nimekuitikia Ee Allaah nimekuitika, nimekuitika Huna mshirika nimekuitika, hakika Sifa njema zote na Neema na Ufalme ni Vyako Huna mshirika."

Mwanamume atasema kwa sauti na mwanamke atasema kiasi cha kumsikia wa pembezoni mwake ikiwa ni wanawake wenzake. Dalili ni Hadiyth ifuatayo ya kutoka kwa baba yake As-Saaib bin Khallaad amesema: Rasuli (صلى الله عليه وآله وسلم) amesema:

**((أَتَانِي جِبْرِيلُ فَأَمَرَنِي أَنْ آمُرَ أَصْحَابِي أَنْ يَرْفَعُوا أَصْوَاتَهُمْ بِالْإِهْلَالِ وَالتَّلْبِيَةِ))**

***((Amenijia Jibriyl akaniamrisha niwaamrishe Maswahaba zangu wapandishe sauti zao katika kuchinja na Talbiyah))***[3]

Anatakiwa mtu kusema *Talbiyah* kila mara khaswa anapofika na kubadilisha kituo. Mfano anapopanda na kushuka kipando wakati wa safari au wakati wa usiku unapoingia na asubuhi kunapopambazuka. Pia

[2] At-Tirmidhiy - *Swahiyh At-Tirmidhiy* (828).
[3] At-Tirmidhiy – Ameisahihisha Al-Albaaniy katika Swahiyh At-Targhiyb wat-Tarhiyb (1135).

Amuombe Allaah (سبحانه وتعالى) Ridhaa Yake ya kupata Jannah na aombe kujikinga kwa Rahmah ya Allaah (سبحانه وتعالى) dhidi ya moto.

Anatakiwa mtu aseme *Talbiyah* wakati wa 'Umrah tokea anapovaa Ihraam yake hadi anapoanza *Twawaaf*. Wakati wa Hajj aseme *Talbiyah* kutokea mwanzo wakati anapovaa Ihraam yake mpaka anapoanza kurusha vijiwe *Jamrat Al-'Aqabah* tarehe 10 Dhul-Hijjah (*Yawm An-Nahr*).

| **Yanayoharamishwa Katika Ihraam** | | |
|---|---|---|
| **Wanaume Na Wanawake** | **Wanaume** | **Wanawake** |
| Wasikate nywele. Hapana ubaya kukuna kichwa au kuchana nywele na ikiwa zitatoka kwa ajili hiyo hakuna ubaya. | Haifai kujifunika kichwa kama kuvaa kofia, kilemba, ghutrah na kadhalika. Ama kujifunika mwavuli kwa ajili ya kujihifadhi jua hakuna ubaya. Pia hakuna ubaya akibeba begi lake kichwani. | Asivae niqaab na glavu. Kuna Ma'ulamaa waliosema kuwa haifai kujifunika uso wake kwa niqaab au chochote kingine ila kama kuna wanaume karibu yake, basi inambidi ajifunike uso wake kwa ghashwah[4] (kuepusha fitnah). |
| Wasikate kucha. Ikikatika kucha na ikiwa inamuudhi hakuna ubaya kuikata. | Asijitie manukato mwilini, au katika nguo zake baada ya kuingia katika Ihraam. Ama kabla ya Ihraam inafaa (kama ilivyoelezwa mwanzo). Vile vile | Hawaruhusiwi kabisa kutia manukato ikiwa kabla ya Ihraam au baada yake. |

[4] Mtandio au shungi jepesi la kufunika uso bila ya kubanika uso.

| | | |
|---|---|---|
| | katika chakula kama kutia zaafarani kwani zaafarani ni katika harufu nzuri. Vilevile ajiepushe na kuoga sabuni iliyo na manukato. Hakuna ubaya ikiwa manukato aliyotia kabla ya Ihraam yamebakia katika nguo zake. | Vile vile katika chakula kama kutia zaafarani kwani zaafarani ni katika harufu nzuri. Vilevile ajiepushe na kuoga sabuni iliyo na manukato. |
| Wasigusane kwa hamu au kubusiana, au kujimai (kitendo cha ndoa). | Asivae nguo zilizoshonwa kama fulana, shati, suruwali, chupi, soksi, viatu na kadhalika.<br><br>Anaruhusiwa kuvaa saa, miwani visaidizi vya kusikia au kuzungumzia. | Avae nguo zake za kawaida ziloshonwa zinazokubalika ki-Shariy'ah. |
| Wasifunge nikaah (ndoa) wala kupeleka posa kwa mwanamke kwa ajili yake au mwenzake. | | |
| Wasivae glavu, lakini hakuna ubaya kufunika mikono kwa nguo yake. | | |
| Wasiwinde, wasikate miti, | | |

| | | |
|---|---|---|
| wasiue wanyama, wadudu. | | |
| Wasifanye maasi yoyote. | | |
| Wasiingie katika mabishano, ugomvi, kutukanana, wala kuongea ya upuuzi n.k. | | |

**Yanayofahamika Sivyo Na Yanayotendeka Kimakosa**

- Wanawake kudhani kwamba lazima kuvaa nguo nyeupe au kijani au aina nyenginezo. Nguo zozote zile zinafaa kuvaliwa, la muhimu ziwe zenye kumstiri na kutimiza masharti ya hijaab.

- Kulazimika kuswali Rakaa mbili baada ya kufanya ghuslu ya kuingia katika Ihraam. Unapokuwa nyumbani huhitaji kuswali bali unaweza kuswali kwa niyyah ya *Sunnatul-Wudhuw*, na ukiwa uko *Miyqaat* ni kuswali *Tahiyyat Al-Masjid*.

- Kutamka *Talbiyah* kwa pamoja, mmoja anasema na wengine wanafuata. Haipasi hivi kwani ni bid'ah. Kila mtu anatakiwa atamke pekee.

- Wanaume kutokujifunika kichwa (kuvaa kofia) baada ya kufanya *ghuslu* kabla ya kuhirimu. Anaweza mtu kuvaa kofia lakini anapofika *Miyqaat* akahirimu hapo asijifunike kitu kichwani.

- Wanawake kutamka *Talbiyah* kwa sauti, khasa pale wanaume wanapotamka katika mabasi. Mwanamke anatakiwa atamke *Talbiyah* yake kwa sauti ya kujisikia mwenyewe tu (moyoni).

- Kudhania kwamba mtu anapoingia katika Ihraam, hawezi tena kwenda kujisaidia msalani au kula. Bali anaweza mtu kwenda haja ndogo au kubwa kisha akafanya wudhuu wake kama anavyofanya kwa ajili ya Swalaah.

- Kudhania kwamba mtu hawezi kubadilisha nguo zake za Ihraam. Unaweza kuoga na kubadilisha nguo, kwani Ihraam ni niyyah na *Talbiyah* na si nguo.

- Wanawake kujifunika uso kwa niqaab na kuvaa glavu. Haifai hivyo isipokuwa kunapokuwa na fitnah ndipo anaruhusiwa kujifunika uso kwa kuangusha mtandio.[5]

- Kujiwekea kivuli juu ya kichwa akiwa katika gari, basi au khema.

- Wanaume kufunika mabega yote mawili kwa shuka ya juu na hivyo kutokuacha bega la kulia kuwa wazi wakati wa *Twawaaf*.

- Baada ya Twawaaf wanaume kuacha mabega wazi wakidhania ni lazima kuwa hivyo nyakati zote.

- Wanaume kukaa ovyo hadi kuonekana sehemu zao za siri kwa vile hawakuwa wamevaa suruwali ya ndani (chupi).

- Wanaosafiri kwa ndege kutokuhirimia ndani ya ndege ikiwa wanaanza manaasik zao kwa 'Umrah.

[5] Rejea Mlango wa 'Yanayohusu Wanawake.'